

# Masharti ya

## ***Kalahari Short Story Competition***

### Kutoka kwa La CENE Littéraire

---

#### **Kipengele cha kwanza – Jina**

Shirika la *La CENE Littéraire* limezindua rasmi mashindano ya uandishi wa fasihi uitwao, "***Kalahari Short Story Competition***".

#### **Kipengele cha Pili - Masharti ya kushiriki**

2.1. Kushiriki katika mashindano ni bure. Shindano hili liko wazi kwa waandishi wote ambao hawajachapisha kitabu. Ikiwemo watu wa mataifa yote licha ya umri au sehemu wanaoishi.

2.2. Kila mshiriki anapaswa kutuma hadithi fupi ambayo haijachapishwa yenye maneno yasiyopungua 2500 na yasiyozidi 3500, katika lugha ya Kiswahili, Kiingereza au Kifaransa.

2.3. Kila hadithi fupi, ni lazima iwe na muktadha ufuatao kutoka kwa riwaya ya Elnathan John, "*Born on a Tuesday*", mshindi wa *Prix Les Afrique 2019*:

"Siwezi kula wala kulala, na wala siwezi kuzuia mikono yangu isitetemeke. Pindi kutakapokucha, nitaondoka mahali hapa"

2.4. Hadithi zitakazotumwa ziwe katika hati ya Microsoft word, mtindo wa Times New Roman, ukubwa wa pointi(fonti) 12 na nafasi iwe 1.0, hii haitajumuisha jina wala sahihi.

2.5. Washiriki wa miswada wanapaswa kupeleka maombi na hadithi fupi zao kupitia baruapepe: **[competition@collection-kalahari.com](mailto:competition@collection-kalahari.com)**

2.6. Idhini iliyoandikwa na kusainiwa na wawakilishi wa kisheria inafaa kuambatishwa pamoja na miswada itayakayotumwa na waandishi wenye umri mdogo.

### **Kipengele cha tatu – Hakimiliki**

3.1. Kwa kutuma miswada, washindi wanakubaliana kuwa hadithi zao zitafasiriwa, zitachapisha na zitasambazwa kupitia njia tofauti na La CENE Littéraire.

3.2. Kwa kushiriki katika mashindano, washindi watawapa La CENE Littéraire haki za umiliki wa hadithi hizo.

3.3. Kwa kushiriki katika mashindano haya, washindi watawapa La CENE Littéraire haki za kipekee za kuchapisha hadithi, kutoa nakala na kuuza kupitia njia tofauti.

### **Kipengele cha Nne – Tuzo na uzingatiaji wa mgao wa Hakimiliki**

4.1. Tuzo tatu zitatumukiwa kwa washindi wa kila lugha. (Swahili, Kiingereza na Kifaransa).

- Mshindi wa kwanza : € 1000
- Mshindi wa pili : € 500
- Mshindi wa tatu € 300

4.2. Washindi watapelewa nakala tano ya antholojia ambazo hadithi zao zitachapishwa. Nakala hizi zinajumuisha kutuzwa kulikotajwa 4.1 ambako kutawakalisha hakimiliki ya kitabu hicho.

### **Kipengele cha tano – Ratiba ya mashindano**

5.1. Hadithi fupi zitapokelewa kuanzia Mei 20, 2020 hadi Agosti 20, 2020.

5.2 Matokeo yatatangazwa kupitia tovuti ya <https://collection-kalahari.com/> mnamo tarehe **20, Oktoba 2020**.

## **Kipengele cha Sita – Masharti ya Jumla**

6.1 Kwa kutuma muswada, itachukuliwa kuwa mshiriki ameafiki masharti yaliyowekwa hapo juu bila pingamizi yoyote.

Flore Agnes NDA ZOA MEILTZ

Rais wa La CENE Littéraire